**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Chuo cha Ualimu Tandala,**
**S.L.P.377,**

**Simu: 0763975752** **NJOMBE.**
**Barua pepe: tandalatc@moe.go.tz**
**Website: www.tandalatc.ac.tz**

**Unapojibu taja:-**
**Kumb.Na TTC/UW/17/151** **12/06/2023**

**Ndugu ………………………………..**
**………………… …………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI/AWALI (GATCE) MWAKA WA MASOMO 2023/2024**

## UTANGULIZI

Tunakupongeza kwa kuchaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia ili kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ya Astashahada ya Ualimu wa Elimu Msingi/Awali (GATCE) katika Chuo cha Ualimu Tandala. **Muda wa mafunzo ni miaka miwili (02).**

## MAHALI CHUO KILIPO NA NAMNA YA KUFIKA

Chuo kipo katika kijiji cha **Tandala Wilayani Makete** (Mkoa wa Njombe) umbali wa kilometa 86.6 toka Njombe Mjini. Ukifika Njombe panda mabasi yanayoelekea Ikonda, kama utafika Njombe jioni baada ya mabasi yanayoelekea Ikonda-Makete kuondoka, uliza nyumba za kulala wageni zilizopo karibu na stendi kwenye ofisi za mabasi-Njombe. Ukifika Ikonda telemka katika kituo cha mabasi ulizia sehemu Chuo kilipo, umbali wa kutoka Ikonda stendi hadi chuoni ni kilomita moja ambapo unaweza kutembea kwa miguu.

## DIRA YA CHUO.

Dira ya Chuo ni “Kutoa Walimu Mahiri wa Astashahada (GATCE) wenye maarifa, ujuzi na stadi wanaoweza kukabiliana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na changamoto mbalimbali za maisha Kisiasa, Kijamii na Kiuchumi” na Moto wa Chuo ni “**Elimu ni Kazi”**

## MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

1. **VIFAA VYA DARASANI**

i) Rimu moja ya karatasi ya A.4. (Multifunctional/photocophier) kwa ajili ya mazoezi na mitihani ya ndani **Kila Muhula na inakabidhiwa ofisi ya usajili** (zinapatikana maduka ya karibu na chuo).
ii) Daftari 15 counter book (four au three quire) kwa masomo utakayosoma.
iii) Mathematical set 1
iv) Kalamu za wino, penseli na rula ndefu.
v) Mkoba nadhifu wa kuchukulia daftari, kalamu na vitabu. ***Ni marufuku*** kwa mwanachuo kuweka daftari, vitabu, rula katika mfuko wa suruali, sketi, katika nguo ulizovaa au mkononi. Mifuko ya plastic, viroba na vibebeo vingine visivyo vya hadhi ya mwalimu ni marufuku darasani.

vi) Kila mwanachuo awe na Muhtasari (Syllabus) wa somo mojawapo linalofundishwa shule za msingi na kwa wale wa awali wawe na Mtaala wenye muhutasari kwa pamoja.

## 2. VIFAA VINGINE (MAHITAJI BINAFSI)

Uwe na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

i) Sahani, Bakuli na Kikombe vya bati **(siyo plastic),** kijiko, na uma kwa ajili ya kulia chakula na ndoo ya ujazo wa lita 10 kwa ajili ya usafi binafsi.
ii) Mablanketi mazito mawili, shuka mbili za **pink kwa wasichana** na **blue bahari kwa wavulana** pamoja na mto wenye foronya unaofanana na rangi ya shuka (Shuka za rangi nyingine hazitaruhusiwa).
iii) Nguo za michezo aina ya track suit rangi ya kijivu za dukani zisizo na kofia **(zisiwe za mtumba).** Bukta na fulana za rangi nyekundu na raba za michezo za rangi mbalimbali.
iv) Uje na mopa moja na fagio moja laini (Soft Bloom) kwa wasichana na kwa wavulana uje na Jembe lenye mpini.
v) Picha mbili za passport size **(za rangi)** zenye background ya blue.
vi) Kila mwanachuo awe na pullneck nyeusi ya kuvalia ndani ya shati la chuo.

## 3. SARE

**Wasichana**

i) Shona suti nyeusi mbili (Sketi iwe kama mchoro namba 1 unavyoonesha).
ii) Shati mbili za light blue mikono mirefu.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi/kawaida.
iv) Soksi nyeupe zisizopungua jozi mbili
v) Tai nyeusi mbili **sio "neck tie**"
vi) Tshirt ya chuo inapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi 15,000/=
vii) Kwa wanachuo waislam wanaruhusiwa kuvaa **hijabu nyeupe na sio rangi nyingine.**


PICHA 1



**Wavulana**

i) Shona suti nyeusi mbli (suruali iwe kama mchoro namba 2 unavyoonesha-urefu wa kugusa kiatu)
ii) Shati mbili za 'light blue' mikono mirefu.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi/kawaida.
iv) Soksi nyeusi zisizopungua jozi mbili.
v) Tshirt ya chuo inapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi 15000/=
vi) Tai nyeusi mbili sio "neck tie"

PICHA 2



*** Mavazi ya mitumba na mishono ambayo hayajaelekezwa hayatakubaliwa/hayatapokelewa**

**Aidha sare za chuo zinapatika kwa mafundi walio karibu na chuo, kwa mawasiliano kuhusu sare na ushoni wasiliana na mkufunzi wa mavazi kwa namba 0744169167 au 0768763731**

**4. MAVAZI MENGINE**

i) Uje na mavazi ya heshima ya kiualimu.

ii) Suruali, sketi fupi, gauni fupi **halitakiwi**. Suruali, Sketi na gauni lenye kubana mwili au kuonekana limegeuzwa au kuangaza halitakiwi.

iii) **Nywele:** Kwa wasichana nywele za bandia hazitakiwi.

***Kwa wavulana:***

*i)* Uje na mavazi ya heshima ya kiualimu

*ii)* Pensi na Suruali aina ya 'jeans', dengrizi ama za kupandisha mpaka tumboni au kushusha chini ya kiuno hazitakiwi.

*iii)* Hutakiwi kunyoa kipara, kiduku au mitindo yoyote inayodhaniwa ni ya kihuni.

*iv)* Masweta au makoti utakayokuwa nayo yawe ya heshima.

**5. ADA YA MAFUNZO**

Ada ya Mafunzo ni shilingi laki nne na elfu hamsini **( Tshs 450,000/= )** kwa mwaka.
**MALIPO YA ADA YANAFANYIKA KWA KUTUMIA NAMBA MAALUM YA MALIPO (CONTROL NAMBA )** ambayo utapewa na Mhasibu mara tu mfikapo chuoni (Au waweza wasiliana na Mhasibu kwa namba **0767285709** ili upewe control number). Malipo haya ya ada yanaweza kufanyika kwa awamu mbili kila muhula Tsh 225,000.00

**6. MICHANGO MINGINE**

| NA. | MCHANGO | MCHANGANUO WA MALIPO | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Huduma ya Kwanza | 10,000 | Kwa Mwaka |
| 2 | Usajili na Kitambulisho | 20,000 | Kwa Mwaka |
| 3 | Serikali ya Wanachuo | 5,000 | Kwa Mwaka |
| 4 | Elimu ya Michezo | 30,000 | Kwa Mwaka |
| 5 | Ulinzi | 30,000 | Kwa Mwaka |
| 6 | Usafi, Mazingira na EK | 20,000 | Kwa Mwaka |
| 7 | Ukarabati | 25,000 | Kwa Mwaka |
| 8 | Kukodisha Godoro | 10,000 | Kwa Mwaka |
| 9 | Bima ya Afya | 50,400 | Kwa Mwaka kwa wasiokua na Kadi za Bima ya Afya |
| **JUMLA** | | **200,400** | |

Fedha yote ya michango ilipwe kupitia akaunti ya Chuo **ya NMB**, namba **60401100008** Jina la akaunti ni **Tandala Teachers' College**. Tafadhali **andika jina la mwanachuo anayelipiwa na si vinginevyo**. Baada ya Malipo mwanachuo anatakiwa kuja na **BANK –PAY–IN SLIP** halisi toka bank sio nakala (Photocopy).

**NB:**

- Chuo hakitapokea **fedha taslim** kutoka kwa wanachuo kwa sababu zozote zile.
- Mwanachuo hatapokelewa iwapo hajakamilisha malipo ya Michango na Ada kama ilivyoelekezwa hapo juu.
- **USITEMBEE/USISAFIRI NA HELA CASH KUEPUKA UTAPELI UWAPO SAFARINI**
- Fedha zikishaingizwa kwenye **akaunti ya Serikali hazitarudishwa**.
- Kila mwanachuo anatakiwa kulipa Tsh 10,000 ya mahafali kwa mwaka.

**7. KABLA YA KUFIKA CHUONI**

Nenda kwa daktari anayetambuliwa na Serikali ili upimwe afya yako, fomu ya kupima afya imeambatanishwa. **Chuo hakina huduma maalumu ya chakula (Special Diet) pia Chuo kinatoa huduma ya kwanza kutokana na michango. Kwa Matibabu zaidi mwanachuo atajigharamia au atatumia Kadi yake ya Bima ya Afya (KUWA NA BIMA YA AFYA NI LAZIMA).**

**8. UTAMBULISHO**

Unatakiwa kuja na **vyeti halisi (SIYO NAKALA)** vifuatavyo:-

i) Cheti cha kuhitimu kidato cha nne/sita, (Leaving Certificate) yenye picha na muhuri wa Mkuu wa Shule uliogongwa juu ya picha yako katika cheti chako.

ii) Result slip inayoonesha matokeo yako na daraja ulilopata (kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania)

iii) Cheti cha matokeo ya mitihani ya kitaifa cha Baraza la Mitihani ya kidato cha nne/sita (Academic Certificate)

iv) Cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) ni lazima ulete, majina yalingane na cheti cha NECTA.

v) Kitambulisho cha Taifa (NIDA)/ namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)

Kutoleta vyeti vilivyotajwa hapo juu kutafanya **USIPOKELEWE.** Vyeti vyako utakabidhiwa mwishoni mwa mafunzo baada ya kusajiliwa na BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA na kukamilisha taratibu zote/kulipa madeni yote ya serikali. **Kuleta vyeti vya bandia au ambavyo sio vyako ni uvunjaji wa sheria za nchi ukibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.**

**9. MAPOKEZI**

Mara ufikapo chuoni ripoti Ofisi ya Usajili kwa utambulisho na kukabidhi vyeti, risiti za benki za michango, na vifaa mbalimbali.

Pamoja na maelezo ya hapo juu, kama upo tayari kusoma katika Chuo hiki utatakiwa kufuata kanuni za Chuo. Ukivunja kanuni hizo utaondolewa chuoni. Aidha ukifika chuoni utapewa maelekezo ya namna ya kuishi chuoni.

Endapo utapata changamoto na kuhitaji msaada Maelezo au Ufafanuzi wasiliana kwa namba zifuatazo
Msajili -0763086245 au 0754348656

**MWISHO**
**Tarehe ya kuripoti chuoni ni tarehe 17/7/2023 ifikapo tarehe 30/7/2022 hautapokelewa.**
**Uongozi wa Chuo Cha Ualimu Tandala unakutakia maandalizi mema.**

**KARIBU CHUO CHA UALIMU TANDALA**

**VEDASTO J KIBYALA**
**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO,
TANDALA CHUO CHA UALIMU,
S. L. P. 377,
NJOMBE—TANZANIA.

***Nakala:*** Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
**DODOMA.**

Mthibiti ubora Mkuu wa Shule,
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
S.L.P. 2288,
**<u>IRINGA</u>**

Afisa Elimu,
Mkoa wa Njombe,
S.L.P. 858,
**<u>Njombe</u>**.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo,
S.L.P. 1,
**<u>MAKETE.</u>**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU TANDALA**
**SHERIA ZA CHUO**

***Hizi ni baadhi ya sharia za chuo na mwanachuo akivunja mojawapo ya sheria zifuatazo ataondolewa chuoni na Bodi ya Chuo itapewa taarifa. (BAADA YA KUSAINI NAKALA MOJA IKABIDHIWE OFISI YA USAJILI)***

1. Mwanachuo mwenye mimba, aliyetoa mimba kwa makusudi au anayejaribu kutoa mimba.

2. Ulevi wa pombe, bangi, sigara au madawa ya kulevya.

3. Mwanachuo kujiingiza kwenye tabia ya uasherati au uzinzi na mtu yeyote yule.

4. Mwanachuo kuacha kuhudhuria vipindi vya masomo kwa idadi iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

5. Mwanachuo kujiamulia kuondoka kulala nje/ eneo la Chuo bila ruhusa.

6. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia nafasi yake au uwezo wake kuwafanya wenzake ama watu wengine wasitii Serikali halali ya nchi au chombo chochote halali cha Serikali katika nchi

7. Udanganyifu wa aina yeyote kama vile kughushi vyeti vya kitaaluma, risiti za malipo ya fedha ( k.m. pay – In – Slip).

8. Mwanachuo kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mlezi wake (mkufunzi/mfanyakazi).

**Jina la mzazi/mlezi ……………………………………Namba ya simu......................................**

***Sahihi ………………………….. Tarehe …………………***

**Jina la mwanachuo .......................................................**

***Sahihi ........................................ Tarehe .....................***

***GOVERNMENT OF TANZANIA***

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**PART A.**
**TO,**
**THE MEDICAL OFFICER,**

……………………………………. From……………………
……………………………………. Date………………………

Mr/Mrs/miss……………………………………

Name in Full.

Please Examine the above named as to him/her physical and mental fitness from a full time Teacher Training Course. The Examination should include the following categories:-

(a) Eye – Sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal diseases
(f) Epilepsy
(g) Necroses
(h) Other serious diseases
(i) Pregnancy

**MEDICAL CERTIFICATE**

**PART B**.

**(To be completed by the Government Medical Officer)**

I have Examined the above named and consider that he/she is physically Fit/ Unfit and mentally fit /unfit for a full time Teacher Training Course.

(a) Eye - Sight………………………………………………………………
(b) Hearing…………………………………………………………………….
(c) Limbs……………………………………………………………………
(d) Speech……………………………………………………………………
(e) Venereal disease…………………………………………………………..
(f) Epilepsy…………………………………………………………………….
(g) Necroses…………………………………………………………………
(h) Pregnancy…………………………………………………………………
(i) Other serious disease……………………………………………………

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU TANDALA**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA CHUO**

**I. MWANACHUO**

Jina la Mwanachuo.........................................................................................................................

Anuani ..................................................................................................................................

Mimi ............................................................................... nimekubali kujiunga na chuo cha Ualimu Tandala. Nimesoma maagizo yote ya chuo kwa umakini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria na taratibu zote za chuo kama nitakavyoelezwa.

Saini ya mwanachuo...............................................................tarehe .............................................

**II. MZAZI/MLEZI**

Mimi.............................................................................................................................................

Mzazi/mlezi wa...............................................................................na. simu......................................

Nimesoma kwa makini maagizo ya chuo yaliyotolewa kwa mtoto/kijana wangu. Nimekubali mwanangu ajiunge na chuo hicho. Naahidi kuwa nitashirikiana na Uongozi wa chuo katika kumkuza na kumlea mwanangu kitabia, kielimu na kimaadili ya Ualimu ili kumfanya awe mwalimu wa mfano katika jamii.

Saini ya Mzazi/mlezi.................................................................................. Tarehe.............................

**NB Mzazi/mlezi hakikisha mwanao/kijana wako amezisoma sheria zote za chuo zilizoambatanishwa kwa umakini mkubwa na kuzitafakari, ndipo usaini fomu hii.**